

Bodi za Magavana

Wanachama wa Benki ya Dunia wanawakilishwa na Bodi za Magavana. Kila nchi mwanachama huteuwa Gavana mmoja na mmoja ambaye ni Gavana wa Kupokezana kulingana na [Articles of Agreement](#) [Vifungo vya Maelewano]. Gavana na Mpokezi, kila mmoja hutumika kwa mda wa miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena. Ikiwa mwanachama wa Benki pia ni mwanachama wa IFC ama IDA, Gavana mteule wa Benki na Mpokezi wakepia hutumika kama viongozi rasmi kama Gavana na Mpokezi katika Bodi za Magavana ya IFC na IDA. Magavana na Wapokezi wa MIGA wanateuliwa kivyao. Kwa kawaida, Magavana hawa huwa ni maofisa wa serikali, kama vile Mawaziri wa Fedha ama Mawaziri wa Maendeleo.

Kulingana na Vifungo, uwezo wote wa Benki umewekwa katika Bodi za Magavana. Kuambatana na sheria za Benki zilizokubaliwa na Bodi za Magavana. Magavana wamepeana uwezo kwa Wakurugenzi Watendaji uwezo wote ambao kulingana na Vifungo haukupatiwa kwa ukamili Magavana.

Magavana wanawakubali ama kuwasimamisha wanachama, wanapunguza ama wanaongeza mtaji wa hisa uliyokubaliwa, wanaamua ugawaji wa pato kamili, wanakagua hati za kifedha pamoja na bajeti, na pia wanatumia uwezo mwengine ambao haukupewa Wakurugenzi Watendaji. Bodi za Magavana hukutana mara moja kwa mwaka katika Mikutano ya Mwaka ya Benki. Kwa kawaida, mikutano hufanyika Washington kila miaka miwili kati ya mitatu na, ili kuonyesha hadhi ya kimataifa ya mashirika kila mwaka wa tatu, mkutano huwa kwenye nchi nyengine mwanachama.

- ▶ [IBRD/IFC/IDA Governors & Alternates](#) [Magavana na Wapokezi wa IBRD/IFC/IDA] (398K)
- ▶ [MIGA Governors & Alternates](#) [Magavana na Wapokezi wa MIGA] (341K PDF)